



FRIEDRICH
EBERT
STIFTUNG

women
transporting the world

Dk. Tessa Wright

MATOKEO YA
SIKU ZA USONI
YA KAZI KWA
WANAWAKE
KATIKA USAFIRI
WA UMMA
MUHTASARI



KUHUSU MWANDISHI

Dk. Tessa Wright ni Msomi katika Usimamizi wa Wafanyakazi katika Kituo cha Utafiti wa Usawa na Utofauti, Shule ya Biashara na Usimamizi, katika Chuo Kikuu cha Queen Mary Mjini London. Amefanya utafiti na kuandika kwa mapana kuhusu usawa kazini, haswa maswala ya jinsia, ujinsia na uungano, hususan katika sekta na ajira zinazotawaliwa na wanaume ikiwa ni pamoja na huduma ya zima moto, ujenzi na usafiri. Ana nia katika mikakati ya kukabiliana na ukosefu wa usawa wa kijinsia kazini, zikiwemo hatua za Vyama vya wa wafanyakazi na kutumika kwa ununuzi wa umma. Yeye ndiye mwandishi wa *Gender and sexuality in male-dominated occupations; Women workers in construction and transport (2016)* iliyochapishwa na Palgrave Macmillan na mhariri wa mratibu, pamoja na Hazel Conley, wa Kitabu cha *Gower Handbook of Discrimination at work (2011)*.

Septemba 2018

SHUKRANI

Ripoti hii iliagizwa na Shirika la Wafanyakazi wa Usafiri wa Kimataifa - International Transport Workers' Federation (ITF). Mwandishi wa ripoti hii alipokea usaidizi muhimu na maoni kutoka kwa Claire Clarke, Naibu wa Afisa wa Wafanyakazi wa Usafiri Wanawake na Usawa wa Jinsia na Jodi Evans, Wafanyakazi wa Usafiri Wanawake wa ITF na Afisaa wa Usawa wa Jinsia, pamoja na mchango wake Victor Figueroa Clark, Mtafiti wa Mikakati wa ITF. Utafiti katika miji hii mitano ulifanywa na watafiti wafuatao: Khemphatsorn Thanapatthamanan (Bangkok); Daniela Gomez na Marina Moscoso, Despacio (Bogota); Rob Rees na Sandra Van Niekerk, Naledi (Cape Town); Patricia Robles Muniz (Mji wa Mexico); na Anne Kamau, Chuo Kikuu cha Nairobi, (Nairobi).

Utafiti ulisaidiwa sana na kushiriki kwa wanawake wa vyama vya wafanyakazi katika semina ya utafiti huko Bogota kutoka SNTT na SintraRecaudo (Colombia); MWU, PUTON, TAWU na RAWU (Kenya); ATM (Mexico) na SRUT na SEETU (Thailand) na pia wawakilishi wa ITF kutoka Afrika, Anna Karume; Su-angcana Tungworachet kutoka bara la Asia; na Andréa Privatti kutoka Amerika ya Kusini.

Utafiti haungewezekana bila hiari ya wafanyakazi wa kike na wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi, waajiri na mashirika ya kiraia katika kila moja ya miji hii mitano, kujitolea na kukubali kushiriki katika mahojiano. Shukrani kwao wote.

#OurPublicTransport

ITF ilizindua mpango wao - 'Usafiri wetu wa Umma' (Our Public Transport) mwaka 2016 kuendesha kampeni ya mifumo ya usafiri wa umma unaofaa walio wengi, wafanyakazi na mazingira. Lengo kuu la mpango huo ni kuratibu shughuli, hatua na miradi ili kuimarisha nguvu na uwezo wa vyaama vya wafanyakazi kupata namna mbadala wa usafiri wa umma kwa msingi wa umiliki na uwekezaji wa umma, hali ya ajira na haki za wafanyakazi wa usafiri walioratibiwa katika vyama stawi vya wafanyakazi.

Kamati ya wafanyakazi wa usafiri wa wa kike wa ITF imeamua kuifanya kampeni hii nguzo ya msingi ya mpango wa wanawake wa ITF. Maswala ya kijinsia na kushirikishwa kwa wanawake na uongozi yanajumuishwa katika kila nyanja ya mpango.

www.ourpublictransport.org

MUHTASARI

NA

MAPENDEKEZO

CHIMBUKO LA UTAFITI

Wafanyakazi wa usafiri wa umma, ambao tayari wameathirika pakubwa na sera za ukoloni mamboleo ambazo zinatishia masharti ya ajira, wanakabiliwa na mabadiliko muhimu kutokana na kuanzishwa kwa teknolojia zilizo na uwezo wa kubadilisha zaidi jinsi ambavyo kazi inafanyika, jinsi kazi inavyosimamiwa na kupangwa. Ripoti hii imeagizwa na Shirikisho la Kimataifa la Wafanyakazi wa Usafiri (ITF) ili kuhakikisha kwamba mahitaji na maswala ya wafanyakazi wa usafiri wa umma yanazingatiwa katika mijadala inayohusu kazi katika usafiri wa umma siku za usoni. Mara nyingi wanawake hufikiriwa tuu kama watumiaji wa usafiri wa umma, bila kuzingatia masuala yanayowakabili wanawake wengi wanaoishiriki katika majukumu mbalimbali katika kazi za usafiri wa umma duniani kote.

Ubaguzi wa kijinsia uliopo miongoni mwa wafanyakazi katika usafiri wa uma unamaanisha kwamba wanawake kwa kawaida hujilimbikizia kazi zenye malipo duni za utawala na huduma za wateja, kukiwemo idadi yao ndogo tu kwenye majukumu ya udereva yaliyo na malipo bora. Kazi zinazofanywa na wanawake zinaweza kuhatarishwa kwa utumiaji wa machine zinazojiendesha zenyewe. Walakini, kunazo pia fursa za aina mpya za kazi zinazoletwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia, lakini pia ni muhimu wanawake wapate mafunzo na ujuzi wanazohitaji ili wafaidike na fursa hizo za ajira.

Upanuzi wa miundombinu ya usafiri wa umma katika nchi zinazoendelea unaweza kutoa fursa za kazi kwa wanawake na wanaume, ikiwemo fursa ya kuhama kutoka kazi za vibarua na kuenda katika kazi za kudumu. Walakini, vyama vya wafanyakazi mara nyingi havihusishwi ipasavyo katika majadiliano ya kuanzishwa kwa maendeleo katika usafiri wa umma na mifumo mingi ya ziada inayotumika sana, kama vile huduma maalum ya

usafiri wa basi yaani Bus Rapid Transit (BRT), inaegemea tu kwa mifumo fulani ya biashara ya ushirikiano wa umma na watu binafsi ambazo huenda zikakosa kutetea haki za wafanyakazi na masharti mzuri ya kazi. Kwa hiyo utafiti huu unalenga miji mitano ambayo inaanza aina mpya ya mfumo wa usafiri wa umma au inapanua hali ya usafiri zilizopo ambazo zina matokeo muhimu kwa kuajiriwa kwa wanawake. Miji hizi tano ni:

- Bangkok, Thailand (upanuzi wa Treni ya Anga na mitandao ya metro);
- Bogota, Colombia (BRT ilianzishwa mwaka 2000);
- Cape Town, Afrika Kusini (BRT ilianzishwa mwaka 2010);
- Mexico City, Mexico (mipango ya kanda ya basi ya umeme); na
- Nairobi, Kenya (awamu ya kwanza ya ufunguzi wa BRT mwaka 2018).

UTARATIBU WA UTAFITI

Ziara maalum zilifanywa na watafiti walioagizwa na ITF katika kila moja ya miji hizo, wakishirikiana kwa karibu na Idara ya Wanawake wa ITF pamoja na mwandishi wa ripoti, na msaada wa ziada kutoka kwa viongozi wa kikanda wa ITF. Mbinu msingi ya kukusanya data zilikuwa ni ukaguzi wa makala ya ushahidi, mahojiano 164 ya ana kwa ana na kwa njia ya simu na wanawake wanaofanya kazi katika sekta ya usafiri wa umma, wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi, waajiri, mashirika ya kijamii na mashirika yasiyo ya serikali, na watunga sera na wanasiasa.

Mchakato wa utafiti ulihusisha warsha ya ushirikiano huko Bogota iliyoandaliwa na ITF na FES, na kuhusisha watafiti wote pamoja na wawakilishi wa vyama vya

wafanyakazi kutoka miji iliyohusishwa katika ripoti pamoja na ofisi kuu ya ITF na wawakilishi wa kikanda. Hii iliwezesha majadiliano ya thamani kuhusu matokeo ya utafiti wa kwanza katika miji hii mitano, ikiwemo mchango wa wawakilishi wa vyama vya wafanyakazi kuhusu matokeo ya utafiti wao na ujuzi wao wa kupanga kampeni za kuwatetea wanawake katika sekta ya usafiri wa umma. Kutokana na warsha, watafiti katika kila mji walitoa ripoti kujumlisha matokeo ya uchambuzi wa makala yao na ziara yao.

KAZI YA WANAWAKE KATIKA USAFIRI WA UMMA

Utafiti ulithibitisha kwamba wanawake wanaendelea kukumbana na ubaguzi wa kijinsia katika sekta ya usafiri wa umma, kwa kulimbikizwa katika ajira hatari zenye mapato duni na kwa wakati mwingine ajira za vibarua. Lakini kumekuwa na mabadiliko, pamoja na idadi kubwa ya wanawake wanaojiriwa katika kazi za usafiri wa umma huko mjini Mexico na Afrika Kusini. Wanawake pia wanapata fursa bora za kuhamia katika sekta zinazotawalwa na wanaume, ikiwa ni pamoja na udereva, katika aina mpya ya mifumo ya usafiri kama vile BRT na mifumo inayopanuka ya metro. Wanawake pia wanavutiwa na mabadiliko ambayo yanawezapatikana kwa kuendesha teksi za jukwaa, ijapokuwa kuna masuala ya usawa na mazingira nzuri ya kazi, ikiwa ni pamoja na hali nzuri ya ajira.

Walakini, wabaguzi wa kijinsia wamekithiri, kuonyesha mtazamo mbaya kuhusu uwezo wa wanawake kuendesha magari au uwezo wao kufanya kazi za usafiri wa umma, na kwa utendaji kupitia utofauti wa hali na masharti ya kazi zinazofanywa na wanawake na wanaume. Kwa upande mwingine, baadhi yao

“ Sikukuu moja ya umma nilichelewa kufika kazini kwa muda wa nusu saa hivi kutokana na ukosefu wa teksi siku hiyo na nikachukuliwa hatuwa za nidhamu .. Sasa inanibidi kuendesha baiskeli yangu saa tisa alfajiri (3:00 am) katika mji ambapo unawezauwawa kwa ajili ya simu yako ya mkononi. Lazima nitoke nje nihatarishe maisha yangu ndiposa nifike kazini haraka.”

Mwanamke mfanyakazi wa S.A.S Recaudo Bogota

walionelea kwamba madereva wanawake ni waangalifu na salama barabarani kuliko wanaume, na pia kuna uwezekano mwingi wao kuwaheshimu abiria. Uwepo wa madereva wengi wa kike pia kulionekana kuwa suluhisho la usalama wa abiria wa kike. Kwa mfano, mjini Mexico, mabasi ya Atenea huendeshwa na madereva wanawake na hudumia abiria wa kike, ilhali Laudrive ni huduma ya teksi ya jukwaa inayohudumia wanawake likiendeshwa na madereva wa kike.

kulingana na maoni ya wafanyakazi, ghasia dhidi ya wanawake na unyanyasaji wa kijinsia kutoka kwa wenzao wa kiume au abiria ni tukio ambalo wanawake wanaofanya kazi kwa usafiri wa umma wanakumbana nao kila mara katika miji yote, pasipo na hatua ya kutosha kuchukuliwa na waajiri na mamlaka kukabiliana na ghasia

za abiria. Unyanyasaji wa kijinsia kwa abiria wanawake pia kulienea, hatua ikichukuliwa kuishughulikia katika ngazi ya serikali za mitaa huko Bogota na mjini Mexico, na vyama vya wafanyakazi kwa kushirikiana na mashirika ya kiraia huko Cape Town na Nairobi.

Masaa za kufanya kazi na kazi za zamu zilichangia wanawake kuhofia usalama wao, na kuwazuia kushiriki katika kazi kadhaa au nyakati fulani, kwa mfano, kuendesha mabasi katika zamu za usiku au teksi za jukwaa wakati wa usiku, kuwasababisha kutofanya nyakati zenye faida zaidi. Wanawake waloiko katika huduma ya wateja na mauzo pia walifanya kazi katika zamu za mapema na usiku lakini uwezekano wa waajiri wao kuwapa usafiri salama kuelekep na kutoka kazini ulikuwa mdogo ukilinganishwa na madereva.

Ukosefu wa vyoo na vipindi mwafaka vya mapumziko inaendelea kuwa tatizo kwa wafanyakazi katika usafiri wa umma na husababisha matatizo ya kipekee kwa wanawake. Baadhi ya madereva na wahudumu katika stesheni waliohojiwa waliripoti ukosefu wa vyoo, na mara nyingi hulazimika kutumia choo kimoja na abiria, bila ya vipindi vya kutosha vya mapumziko ili kutumia vifaa hivyo. Katika tukio nyingine, ukosefu wa vyoo uliaminika kuchangia maambukizi ya njia ya mkojo.

KUANZISHWA KWA TEKNOLOJIA MPYA

Baadhi ya ubunifu wa kiteknolojia, kama zile mashine za kiotomatiki za kuuza tiketi, zimesababishia wafanyakazi wengi kupoteza ajira, hasa wanaofanya kazi za vibarua. Hata hivyo, iwapo wanaoathiriwa na teknolojia mpya ni wanachama wa vyama vya wafanyakazi, mkataba wa uhamisho ulimaanisha kwamba wauzaji wa tiketi,

kwa mfano, walihamishwa kwenda ofisini au kuhudumu kama wasaidizi kwenye mashine za tiketi, na katika visa vingine kuboresha hali ya kazi.

Uwezekano mkubwa wa kuendelea kuwekwa kwa mashine za mauzo ya tiketi na zile za kukusanya nauli ungalipo katika miji yote, ijapokuwa vikwazo vipo kama vile matatizo ya teknolojia, biashara na pia siasa. Mahojiano na wafanyakazi wa kike katika kazi za kuuza tiketi na huduma za wateja yalionyesha kwamba abiria hupendelea mawasiliano na binadamu kuliko huduma za mashine, ambazo mara nyingi hufanya kazi polepole au vibaya. Kwa kweli mashine duni inasababishia abiria ghadhabu na kuchangia kuvurugwa kwa wafanyakazi.

Fursa ya mafunzo ni muhimu ili kuhakikisha kwamba wanawake wanapata nafasi za ajira mpya iwapo miundombinu ya usafiri inaanzishwa au kuboreshwa pamoja na mafunzo ili kupata leseni za udereva au kuendesha mifumo mpya ya kiteknolojia. Katika mifano mingine kama ile ya 'CAPE TOWN BRT', uanafunzi au taratibu ya mafunzo yanayofadhilwa yalitumika kufundisha wanawake ili wapate leseni za udereva na kuongeza idadi yao katika uendeshaji wa mabasi.

Ijapokuwa kunazo uwezekano wa wafanyakazi wanawake kufaidika kutokana na kuanzishwa kwa mifumo ya

“ Usafiri wa umma sio nzuri kwa wafanyakazi wa kike na watumiaji, na abiria pamoja na wafanyakazi hukumbana na mahangaiko.”

Mwakilishi mwanamme wa chama cha wafanyakazi, Nairobi

BRT, aina ya ufadhili ambayo chini yake mfumo huu unaendesheka unasisitiza ushirikiano wa umma na kibinafsi, unaosababisha ushindani kati ya makampuni yanayoendesha magari na kutengwa wa utawala wa mamlaka ya mitaa na udhibiti wa uendeshaji wa huduma. Hii kwa kawaida huzuia usimamizi wa kutosha wa sheria na masharti ya wafanyakazi katika kila kampuni, na mara nyingine, ilisababisha sheria na masharti mabaya ya udereva ikilinganishwa na makubaliano ya awali ya vyama vya wafanyakazi. Hivyo basi, huenda wanawake wanaajiriwa katika ajira mpya ya udereva chini ya masharti mbaya kuliko awali.

KAZI YA JUKWAA KATIKA USAFIRI WA MIJI

Kwenye utafiti huu, makampuni ya tekisi zisizo za jukwaa yanapanuka katika miji mingi, ijapokuwa Uber waliondoa huduma zao nchini Thailand mwaka 2018, kufuatia azimio ya serikali kwamba tekisi za jukwaa hazijasajiliwa ipasavyo nchini humo. Msimamo wa kisheria wa waendeshaji wa tekisi za jukwaa huko Bogota ni badilifu, ambako jukwaa inatambulika kisheria lakini madereva wanaoitumia hufanya kazi kinyume na utawala wa udhibiti. Hii ni kikwazo kwa madereva wa kike ambao hawawezi toa lalama kisheria, au kuuliza usaidizi wa polisi wanapo kumbana na hatari kutoka kwa abiria. Hali ya kutodhibiti huduma pia inazuia vyama vya wafanyakazi kuwaratibu madereva wa jukwaa.

Utafiti huu unaunga mkono madai kwamba uendeshaji wa tekisi za jukwaa unaweza wapa wanawake fursa za ajira zisizowazuia kusawazisha kazi pamoja na majukumu mengine kama kushugulikia familia zao au masomo. Hata hivyo, faida hizi zinaweza kuwepo kwa wanawake ambao hawaitegegemei tu kazi hii kama mapato

ya kipekee, au wale ambao wana gari zao binafsi. Hivyo basi, uwezekano wa unyanyasaji ni mkubwa kwa wanawake masikini ambao wanalazimika kulipia magari wanayotumia, au wanaolazimika kufanya kazi kwa muda mrefu sana ili wapate mapato ya kutosha - hasa katika miji yenye ushindani mkubwa kutoka kwa makampuni mengi ya jukwaa na uzito wa mapato.

Hatari za ghasia na unyanyasaji wa kijinsia zinaweza kuwa kizuizi kwa madereva wa kike, na matokeo yake ni kwamba wanawake hujaribu kuepuka kufanya kazi katika maeneo fulani na nyakati ya usiku, hivyo basi kupoteza baadhi ya kazi zenye faida nyingi. Teknolojia inawezatumika kuwatahadhari madereva wa kike dhidi ya wateja hatari, au kuitisha msaada kutoka kwa madereva wengine, na kunaweza kuwa na mengi yanayoweza kutekelezwa ili kuendeleza uthabiti, programu au mifumo yapatikanayo kwa urahisi ili kuhakikisha kwamba madereva wana uhakika kwamba watapata msaada wa haraka wanapokabiliwa na hatari.

MIKAKATI YA VYAMA VYA WAFANYAKAZI KWA WANAWAKE KATIKA USAFIRI WA UMMA

Wanawake wengi wanaofanya kazi katika usafiri wa umma wanapanga miongoni mwa vyama vyao vya wafanyakazi kulinda kazi na kuboresha sheria na masharti ya kazi yao wanawake wanapokuwa katika nafasi za uongozi na kuna hatua wazi kuhusu masuala ya kijinsia. Kwa mfano, SintraRecaudo huko Bogota imefaulu katika kuratibisha wafanyakazi wanaouza tiketi kwenye mfumo wa BRT, kwa kushughulikia malalamishi yao kuhusu sheria na masharti, usalama wao na kuachishwa kazi. Wafanyakazi wa matatu pamoja na wale wa tekisi za

“ *Mimi ni muungwana kwa mke wangu, binti yangu na hata kwa wasichana barabarani, lakini katika njia ambayo mimi huendeshea ... wanawake wanafahamu jinsi mazingara ya wanaume yalivyo, ingawaje wanataka kufanya kazi hapa ... Si mimi ndie napaswa kubadilisha tabia ... walitaka kufanya kazi hapa, hawafanani na wanawake wengine. Najua hao ni wanawake, lakini si kama wengine, umeelewa? Ikiwa wanaitaka, kuja upate. ”*

Dereva mewanamme wa Mabasili, Mjini Mexico

jukwaa wamejiunga na PUTON huko Nairobi. Wanawake wamejitwika jukumu kubwa katika kupinga hatua ya Uber kuwalemeza baada ya kuhudhuria mkutano mmoja wa muungano, katika shirika la wafanyakazi wa jukwaa katika PUTON na kwa kujadiliana na serikali na wadau wengine kushughulikia masuala ya kudhibiti bei, hali ya ajira na usalama.

Wanawake katika vyama vya ushirika pia wameshirikiana kwa ufanisi na wanaharakati wa jamii na abiria, kwa mfano katika kampeni ya ATM huko mjini Mexico kuokoa mabasili, kuonyesha umaarufu wao na watumiaji. Zaidi ya hayo, vyama vya ushirika vimetengeza uhusiano na mashirika yasiyo ya serikali kwenye kampeni juu ya

“Sina kitanda cha kupumzikia ndani ya treni. Inanibidi nilale kando ya choo na kutumia lesa kama pazia ili nijisitiri kutoka kwa abiria.”

Mwanamke anayekaribisha abiria katika treni, Bangkok

unyanyasaji wa kijinsia huko Cape Town na Nairobi, kuonyesa uwezo zaidi wa ushirikiano na mashirika ya jamii na abiria, kuimarisha kampeni za vyama vya wafanyakazi juu ya masuala yanayoathiri kwa pamoja wanawake wafanyakazi wa usafiri wa umma na abiria, kwa faida ya makundi haya yote.

Zipo changamoto nyingi kwa vyama vya wafanyakazi kuratibu wafanyakazi wa jukwaa, kutokana na hali ya ajira zao tofauti na ajira zisizo salama. Hata hivyo ripoti imeonyesha mifano ya kuratibu zilizofaulu huko Cape Town na Nairobi, ambapo wafanyakazi wa jukwaa wamejiunga au kufanya kazi kwa karibu na vyama vya usafiri wa umma vilivyopo. Kwa mfano, madereva huko Cape Town wameunda shirika lao wenyewe liitwalo Uber Drivers Guild. SATAWU iliwaunga mkono madereva kuulizia thibitisho kwamba hali yao ya kisheria kama waliojiajiri wenyewe, kesi ambayo walipoteza mahakamani kwa sababu za kistadi, lakini ilidhihirisha mfano muhimu wa ushirikiano katika sekta hii. Ni dhahiri kwamba msingi wa kisheria ya kazi za kujiajiri miongoni mwa wafanyakazi wa jukwaa utaendelea kupingwa katika miji mingine, kwa usaidizi wa vyama vya wafanyakazi.

Vyama vya Wafanyakazi katika tukio nyingine bado havifanyi vyakutosha ili kuwavutia au kuwatetea wanawake wafanyakazi wa usafiri wa umma, kukuwepo

baadhi ya waliohojiwa wanaoamini kwamba vyama vya wafanyakazi havichukulii visa vya unyanyasaji wa kijinsia kwa umuhimu vinaporipotiwa, hivyo kuwazuia wanawake kujiunga navyo. Mikakati ya vyama vya wafanyakazi kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na fujo kwa wafanyakazi wa kike inahitaji kukuzwa zaidi, na kuwekwa bayana mno na kutekelezwa kwa haki ili kuwaweka moyo wanawake wafanyakazi wa usafiri. Mifano mingine kwa udogo ya mafunzo ya vyama vya wafanyakazi na kufahamisha watu juu ya masuala ya unyanyasaji na ubaguzi wa kijinsia yalionyeshwa.

Wanawake kadhaa ambao ni viongozi katika vyama vya wafanyakazi na wanaharakati walishiriki katika utafiti huu, wakidhihirisha kwamba kukiwa na wanawake katika nafasi za uongozi chamani, masuala yanayowakabili wanawake wafanyakazi wa usafiri huibuka na kushughulikiwa vilvyo na chama. Kule kuonekana wazi kwa viongozi wanawake pia kunachangia kuajiriwa kwa wanawake wafanyakazi wa usafiri wa umma, jinsi inavyodhihirishwa na mfano wa SintraRecaudo huko Bogota.

MAPENDEKEZO

- Kampeni ya kuhakikisha kwamba vyama vya wafanyakazi wanashirikishwa kama wadau muhimu katika mashauriano juu ya miundombinu yote ya usafiri wa umma na upanuzi wa mifumo iliyopo katika zile hatua za mwanzo za majadiliano, na kwamba hatia za kijinsia zinajumuishwa, na kwamba tathmini za athari za kijinsia yanawekwa tayari na hatua sawia zinachukuliwa.
- Kampeni ya kuhakikisha kwamba vyama vya wafanyakazi wanashirikishwa kama wadau muhimu katika mashauriano juu ya miundombinu yote ya usafiri wa umma na upanuzi wa mifumo

iliyopo katika zile hatua za mwanzo za majadiliano, na kwamba hatia za kijinsia zinajumuishwa, na kwamba tathmini za athari za kijinsia yanawekwa tayari na hatua sawia zinachukuliwa.

- Jadili kujumuishwa kwa masharti katika mikataba kati ya mashirika ya usimamizi wa BRT na makampuni endeshi yanayoshughulikia heshima kazini na haki za ajira, kama vile viwango vya chini zaidi vya mshahara, masaa, vifaa na pamoja na hatua za usawa wa kijinsia, kama vile sera za unyanyasaji wa kijinsia, na fursa ya vyeo na mafunzo.
- Kampeni ya kuhakikisha kwamba miundombinu ya usafiri wa umma zinajumuisha vifaa vya kutosha kwa wafanyakazi na abiria, kama vile vyoo na maji safi ya kunywa.
- Kuhakikisha yakwamba mikataba ya uhamishaji na miongozo ya sera juu za urekebishaji wa kazi pia yanalinda kazi ambazo hufanywa na wanawake, kama vile kazi za tiketi, na sio tu madereva.
- Kuangazia ushahidi kwamba abiria wanapendelea kuwasiliana na binadamu kuliko mashine, pamoja na mapendekezo kutoka kwa shirika la ukaguzi na usimamizi wa usafiri (yaani Veeduria huko Bogota) juu ya haja ya wafanyakazi zaidi katika ukusanyaji wa tiketi na huduma kwa wateja na hatari za usalama wa abiria zinazotokana na kule kupunguza wafanyakazi (unganisha na kufanya kazi ili kuzuia unyanyasaji wa kijinsia wa abiria wa kike).
- Kujadili vyeo, mafunzo na fursa za kuendeleza mafunzo zaidi kuwasadia wanawake wa umri zote wapate ajira za malipa ya juu, kama vile udereva, unyapara na nafasi za usimamizi, na majukumu yanayoundwa na teknolojia hizi mpya.
- Kujadili masaa ya kazi na mitindo ya zamu yanayoratibisha majukumu ya wanawake na wanaume katika familia zao, na kushughulikia hatari za usalama wa awamu zile za mapema na za usiku, kwa mfano kwa kuwapa wafanyakazi usafiri kuelekea na kutoka makazini.
- Kuanzishwe sera na taratibu za kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia uliofanywa na wanachama wa vyama vya wafanyakazi; kuwekwe wazi sera za wanachama wa vyama vya wafanyakazi na wafanyakazi wa usafiri wa kike ambao sio wanachama; wafundishe wanachama kuhusu sera na wawakilishi wa vyama jinsi ya kusaidia kesi ya unyanyasaji wa kijinsia.
- Kuendelezwe kampeni kwa kushirikiana na waajiri kukabiliana na ujeuri wa abiria, kutengezwe uhusiano kati ya utoaji wa mazingira salama kwa abiria na wafanyakazi wa kike; na kujengwe miungano na mashirika yasiyo ya serikali kukampeni za kukomesha ujeuri wa kijinsia na / au usafiri wa umma salama.
- Kukuza uongozi wa wanawake katika vyama vya wafanyakazi kwa njia za miundo ya wanawake, mitandao na mafunzo ambayo yanaendeleza uwezo wa wanawake wa vyama vya wafanyakazi kuhusika na kutekeleza majukumu ya uongozi.
- Kampeni ya sera za kusaidia kushughulikia teknolojia na ukosefu wa usawa wa kijinsia - katika ngazi ya maeneo ya kazi, ngazi ya serikali na uratibu, ikiwa ni pamoja na kutumia fursa kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, na kuhakikisha kwamba mazungumzo kama hayo yanaelezea wazi haki za kikazi na ukosefu wa usawa wa kijinsia.

KUHUSU ITF

Shirikisho la Wafanyakazi wa Usafiri wa Kimataifa (ITF) ni shirikisho la kidemokrasia, la hiari linaloongozwa na washirika ambao ni vyama vya wafanyakazi 670 katika nchi 147, vinavyowakilisha wanawake na wanaume milioni 19.7 wanaofanya kazi katika sekta zote za usafiri. ITF inathamini Kampeni za kutetea haki za wafanyakazi wa usafiri, usawa, na haki.

Idara ya wanawake ya ITF hufanya kazi na kamati ya wafanyakazi wa kike wa usafiri ya ITF, kusaidia washirika wa ITF kuratibu na kuhamasisha wafanyakazi wengi wa kike wa usafiri na kuongezea ushawishi wetu kimataifa na nguvu katika maeneo yetu ya kazi za safiri. Lengo letu ni kuimarisha sauti yao ya pamoja kupata masharti bora kwa wafanyakazi wa usafiri wa kike ulimwenguni kote. Masuala muhimu ni pamoja na ubaguzi wa kijinsia kazini, upatikanaji wa mishara bora na ajira nzuri, na haki ya kufanya kazi bila udhia, unyanyasaji wa kijinsia na kushurutishwa kutenda ngono.

www.itfglobal.org

KUHUSU FES

Friedrich-Ebert-Stiftung (FES) ndilo shirika la zamani kabisa la kisiasa nchini Ujerumani iliyo na demokrasia ya kijamii asili tangu mwanzo wake mwaka 1925. Shirika hili linawajibu wa kuundwa kwake na lengo lake kwa urithi wa kisiasa wa jina lake Friedrich Ebert, Rais wa kwanza wa Ujerumani kuchaguliwa kidemokrasia. Kazi za shirika letu la kisiasa zinalenga mawazo na maadili ya msingi ya demokrasia ya kijamii - uhuru, haki na mshikamano. Hii inatuunganisha na demokrasia ya kijamii na vyama huru vya ushirika. Kama taasisi isiyo ya faida, tunapanga kazi yetu kwa uhuru na kwa kujitegemea.

www.fes-london.org



**FRIEDRICH
EBERT
STIFTUNG**

